Mungu Wetu Yuko Wapi?

na

Ellis P. Forsman

Mungu Wetu Yuko Wapi?

na

Ellis P. Forsman

Oktoba 17, 2011

Mungu Wetu Yuko Wapi?

Zaburi 42:

Zaburi 42:3, "*Machozi yangu yamekuwa chakula changu mchana na usiku, pindi wanaponiambia mchana kutwa, yuko wapi Mungu wako.*"

Zaburi 42:10, "*Watesi wangu hunitukana mith*ili *ya kuniponda mifupa yangu, pindi wanaponiambia mchana kutwa yupo wapi Mungu wako?*

Lakini Mungu wetu yuko wapi?

Yuko juu yetu (anatutazama)

Imeonyeshwa kwa kupaa kwake Kristo.

Marko 16:19, "*Basi Bwana Yesu baada ya kusema nao, akachukuliwa juu mbinguni, akaketi mkono wa kuume wa Mungu.*"

Anatazama juu yetu.

Math. 6:25-34, "*Kwa sababu hiyo nawaambieni msisumbukie maisha yenu, mle nini au mnywe nini; wala miili yenu mvae nini. Maisha je! Si zaidi ya chakula, na mwili zaidi ya mavazi? Waangalieni ndege wa angani, ya kwamba hawapandi wala hawavuni, wala hawakusanyi ghalani; na Baba yenu wa mbinguni huwalisha hao. Ninyi je! Si bora kupita hao? Ni yupi kwenu ambaye akijisumbua aweza kuongeza kimo chake hata mkono mmoja? Na mavazi, ya nini kuyasumbukia? Fikirini maua ya mashamba, jinsi yameavyo; haya fanyi kazi, wala haya sokoti name nawaambia, ya kwamba hata Sulemani katika fahari yake yote hakuvikwa vizuri kama mojawapo la hayo. Basi, ikiwa Mungu huyavika hivi majani ya kondeni, yaliyopo leo na kesho hutupwa kalibuni, je! Hatazidi sana kuwavika ninyi, enyi wa imani haba? Msisumbuke, basi, mkisema, Tule nini? Au Tunywe nini? Au Tuvae nini? Kwa maana hayo yote mataifa huyatafuta; kwa sababu Baba yenu wa mbinguni anajua ya kuwa mnahitaji hayo yote. Bali utafuteni kwanza ufalme wake, na haki yake; na hayo yote mtazidishiwa. Basi msisumbukie ya kesho; kwa kuwa kesho itajisumbukia yenyewe. Yatosha kwa siku maovu yake.*"

Mawazo yake na njia zake zi juu zaidi yetu.

Isa. 55:8-9, "*Maana mawazo yangu si mawazo yenu, wala njia zenu si njia zangu; asema BWANA. Kwa maana kama vile mbingu zilivyo juu sana kuliko nchi, kadhalika njia zangu zi juu sana kuliko njia zenu, na mawazo yangu kuliko mawazo yenu.*"

Yuko chini yetu (kutuinua juu)

Mikono yake hututegemeza.

(Musa akiongea kuhusu Waisraeli) Kumbukumbu 33:27, "*Mungu wa milele ndiye makazi yako, na mikono ya milele I chini yako. Na mbele yako amemsukumia mbali adui; akasema angamiza.*"

Anawainua wenye haki.

- Zaburi 37:17, "*Maana mikono ya wasio haki itavunjika, bali BWANA huwategemeza wenye haki.*"
- Ayubu 40:8-9, "*Je hata hukumu yangu utaibatilisha? Utanitia mimi hatiani, upate kuhesabiwa haki? Au je! Wewe una mkono kama Mungu? Waweza kutoa ngurumo kama yeye?*

Yuko mbele yetu (anatuongoza)

Yeye ni kiongozi wetu.

Zaburi 48:14, "*Kwa maana Mungu huyu ni Mungu wetu milele na milele: atakuwa kiongozi wetu hadi kufa.*"

Mfuate yeye.

1 Wafalme 18:21, "*Naye Eliya akawakaribia watu wote akanena, mtasitasita katika ya mawazo mawili hata lini? BWANA akiwa ndiye Mungu mfuateni, bali ikiwa Baali ni Mungu, haya mfuateni yeye. Wale watu hawakumjibu neno.*"

Yuko nyuma yetu (kututia moyo)

Kunasauti nyuma yetu.

Isa. 30:21, "*Na masikio yako yatasikia neno nyuma yako likisema, Njia ni hii, ifuateni, mgeukapo kwenda mkono wa kulia, na mgeukapo kwenda mkono wa kushoto.*"

Yuko katika mkono wetu wa kulia (pa kukaa kwetu)

Tusije tukaondoshwa.

Zaburi 16:7-8, "*Nitamhimidi BWANA aliyenipa shauri, naam mtima wangu umenifundisha usiku. Nimemweka BWANA mbele yangu daima, kwa kuwa yuko kuumeni kwangu sitaondoshwa.*"

Paulo hakuruhusu chochote kumuondosha.

Matendo 20:24, "*Lakini siyahesabu maisha yangu kuwa kitu cha thamani kwangu kama kuumaliza mwendo wangu na huduma ile niliyopewa kwa Bwana Yesu, kuishuhudia Habari Njema ya neema ya Mungu.*"

Ametuzunguka (kinga yetu)

Kama milima ilivyoizunguka Yerusalemu.

Zaburi 125:2, "*Kama milima ilivyozunguka Yerusalemu, ndivyo BWANA anavyowazunguka watu wake, tangu sasa na hata milele.*"

Kama ukuta wa moto umetuzunguka.

Akizungumzia Yerusalemu mpya, kanisa. Zekar. 2:5, "*Kwa maana mimi asema BWANA nitakuwa ukuta wa moto kuuzunguka pande zote, nami nitakuwa huo utukufu ndani yake.*"

Tunapaswa kuwa kwake.

Yohana 15:1-6, "*Mimi ndimi mzabibu wa kweli, na Baba yangu ndiye mkulima. Kila tawi ndani yangu lisizaa huliondoa; na kila tawi lizaalo, hulisafisha ili lizidi kuzaa. Ninyi mmekwisha kuwa safi kwa sababu ya lile neno nililowaambia. Kaeni ndani yangu, nami ndani yenu. Kama vile tawi lisivyoweza kuzaa peke yake, lisipokaa ndani ya mzabibu; kadhalika nanyi msipokaa ndani yangu. Mimi ni mzabibu ninyi ni matawi, akaaye ndani yangu nami ndani yake, huyo huzaa sana; maana pasipo mimi ninyi hamwezi kufanya neno lo lote. Mtu asipokaa ndani yangu, hutupwa nje kama tawi na kunyauka; watu huyakusanya na kuyatupa motoni yakateketea.*"

Yu pamoja nasi (mfariji wetu)

Hatuitaji kuogopa.

Isa. 41:10, "*Usiogope kwa maana mimi ni pamoja nawe; usifadhaike kwa maana mimi ni Mungu wako; nitakutia nguvu, naam, nitakusaidia, naam, nitakushika kwa mkono wa kuume wa haki yangu.*"

Kaa katika mafundisho na Kristo atakaa ndani yetu.

2 Yohana 1:9, "*Kila apitaye cheo wala asidumu katika mafundisho ya Kristo, yeye hana Mungu. Yeye adumuye katika mafundisho hayo, huyo ana Baba na Mwana pia.*"

Yu ndani yetu (kutupatia tumaini)

Tumaini la utukufu.

Wakol. 1:27, "*Ambao Mungu alipenda kuwajulisha jinsi ulivyo utajiri wa utukufu wa siri hii katika mataifa, nao ni Kristo ndani yenu, tumaini la utukufu.*"

Hitimisho.

Yeye ni yote kutuhusu sisi.

Waef. 4:6, "*Mungu mmoja, naye ni Baba wa wote, aliye juu ya yote na katika yote na ndani ya yote.*"